

Maisha Yako Mapya



na Ev. Dr. Dana Morey



na Ev. Dr. Dana Morey

Your New Life
English
Copyright ©2020 A Light to the Nations

All rights reserved.

No part of this publication may be reproduced or transmitted in any form or by any means, electronic or mechanical, including photocopying, recording, or any information storage and retrieval system, without permission in writing from the author and publisher.

Scripture taken from the HOLY BIBLE,
NEW INTERNATIONAL VERSION®,
and NEW LIVING TRANSLATION
Copyright © 1973, 1978, 1984 Biblica.

Used by permission of Zondervan. All rights reserved.

The “NIV” (New International Version) and “NLT” (New Living Translation) trademarks are registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica. Use of either trademark requires the permission of Biblica.

Cover & interior design by PixelGraphics

Published by
A LIGHT TO THE NATIONS

This booklet has been distributed
free of charge during
A LIGHT TO THE NATIONS
GOSPEL CAMPAIGN
and is
NOT FOR SALE

Hongera sana!

Hongera sana! Umefanya uamuzi wa muhimu na ajabu sana katika maisha yako. Uameamua kumuamini Yesu Kristo na kumpokea kuwa BWANA na mwokozi wako. Umekuwa mwana wa MUNGU, na dhambi zako zimesamehewa na umeanza maisha yote mapya. Hii ni hatua ya kwanza kuelekea maisha mazuri ya kuwa mfuasi wa kweli wa YESU Kristo.

Hii inakwenda kubadili kila kitu!

Mpendwa rafiki yangu, nina furaha sana juu yako, lakini siko peke yangu, Biblia inasema malaika huko mbinguni wanashangilia kwa sababu umemgeukia MUNGU (Luka 15:10). Maisha yako tayari yameanza kubadilika. Mambo ya zamani hayako tena kwako. Hatima yako itabadilika. Mungu amekuleta kwenye familia yake nzuri na ya kustaajabisha na mambo usiyotegemea ameyaandaa kwaajili yako.

Sababu iliyonifanya kuandika kichwa cha kijitabu hiki ni kukusaidia kuwa rafiki wa karibu na mfuasi wa YESU. Ni maombi yangu kuwa utakisoma kwa umakini na kuchukua ushauri nitakaokupatia hapa. Kurasa hizi chache zitakufunulia siri kubwa ya

kukufanya kuwa imala katika mahusiano yako na MUNGU. Nitakwambia mambo yatakayokufanya ukue na mengine yatakayokulinda ili usiingie katika njia mbaya. **Ninakushauri kwamba usome kitabu hiki mala nyingi zaidi na hata upigie msitari vipengele muhimu kwako, waweza kuungana katika kikundi ili kukipitia kwa pamoja. Hapo mwishoni kuna maswali unayopaswa kuyajibu yatakayoweza kukupanua uelewa wako juu ya ukweli huu. Utapata majibu yote ya maswali yote kupitia kurasa za kitabu hiki. Umeanza safari ndefu ya maisha yako nami nitaendelea kukuombea sana.**

Hiki ndicho kilichotokea ulipomwamini YESU

Kitu cha kwanza unapaswa kujua ni kile kilichotokea ulipoomba maombi yako ya kumpokea YESU “Muda umefika” Yesu alisema “ufalme wa MUNGU umekaribia, tubuni na kuiamini injili” (Marko 1:15). Hicho ndicho ulichokifanya! **Uligeukia mbali na dhambi na kumgeukia Mungu (toba) na uliziamini habari njema. Habari njema ni hizi YESU alikufa msalabani na alifufuka kutoka kwa wafu ili kulipa deni ya dhambi zetu na kutupa uzima wa milele.** Alifanya hivi ili usamehewe dhambi zako na upewe haki zote za kuwa mwana wa MUNGU, ulipoamini habari njema na kumwomba yesu akusamehe dhambi zako, aliingia ndani ya moyo wako na kukufanya kiumbe kipya, biblia inasema “hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama yamekuwa mapya” (2 COR 5:17). Acha niseme hii tena, umepewa MAISHA MAPYA Mungu amesikia maombi yako na ameahidi hivyo. Yohana

1: 12 “bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake”. **Sasa umekuwa mwana wa Mungu.** Kila kitu kwenye maisha yako kimeanza upya. Na hata ukifa hutakuwa tena na deni la dhambi, badala yake utaurithi uzima wa milele na Yesu Kristo milele. Haleluya umepewa zawadi ya uzima wa milele. Je huoni kuwa tuna kila sababu ya kumshangilia Mungu kwa mambo aliyotutendea?

“...kalama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo yesu BWANA wetu.”

Sasa, ni muhimu sana wewe kutambua. Haya maisha mapya ni zawadi ya bure! Hukujisumbua kwa lolote ili kuipata zawadi hii. Mungu hakukupa uzima wa milele kwa sababu ya mambo mazuri uliyonayo au mambo mazuri uliyofanya. “kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu, wala si kwa matendo, mtu awaye yote asijisifu” (WAEF 2:8,9). Biblia iko wazi kwamba si matendo yako mazuri yaliyokufanya uokolewe, Mungu alikuokoa kwani anakupenda, na Mungu hakusubiri uwe mtakatifu ili akuokoe. Biblia inasema “tulipokuwa tungali na dhambi, Yesu alitufia” (Warumi 5:8)

Mungu alikuokoa kwa neema.

Neema ni Baraka kwa

kutokustahili. Yesu alikufa kwenye msalaba wa Warumi ili akupe neema hii. Ninapenda nikueleze tena. Mungu alifanya

“...Karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu”

hivi kwasababu yeye ni mwema na anakupenda. Yeye ni Mungu wa neema na kushangaza na alihitaji kusamehe dhambi zako ilawe na mahusiano mazuri na wewe.

Wewe ni mwana wa Mungu. Wewe ni wake. Kila kitu kwenye maisha yako kimeanza upya.

Ni muhimu sana uelewe kipengele hiki kifuatacho. Kwasababu ya kile ambacho Yesu alikifanya, **UMESAMEHEWA KABISA!** Mungu alisema, *“kwasababu nitawasamehe maovu yao, na dhambi zao sitazikumbuka tena”* (Waebrania 8:12). Mungu amekusamehe kwa mambo yote mabaya uliyotenda, hata dhambi utakazozifanya. Amezizika kwenye kina kirefu cha bahari. Zimetupiliwa mbali na kusahaulika kabisa. Hatazileta kwako tena. Wewe ni safi mbele za uso wa MUNGU. Anapokutazama anakuona mtoto anayekupenda na aliyekufilia. Hebu hiyo ikuingie kwenye akiri yako. Unaweza kuanza kuishi kama mtu aliye mpya. Wewe ni safi, ni mtakatifu na mwenye haki! Hata kama hujioni mtakatifu, Mungu anasema, kwa sababu ya Yesu wewe ni mtakatifu **ukitenda dhambi tubu, mwambie umekosea na mshukuru kuwa Yesu alilipa deni ya dhambi zako. Omba maombi haya sasa hivi. Omba kwa sauti sasa na omba kwa shukrani**

“mpendwa baba yetu wa mbinguni, NAKUSHUKURU! asante kwa kumtoa Yesu kulipa gharama ya dhambi. Ahsante kwa maana umesogeza roho yangu kwako. Asante kwakunipa imani ya kukuamini asante

kwa maana mimi ni mwanao. Nashukuru kunisamehe asante kwamba mimi ni safi na mkamilifu mbele za macho yako, sante kwakuwa mimi ni mfuasi wa YESU Kristo” amina.

SOMO LA 1

Kilitokea nini ulipomwamini Yesu?

1. Kitu gani cha thamani utakipata ukishasoma kitabu hiki?

2. Ulifanya nini kuupokea uzima wa milele?

(MARKO 1:14,15) _____

3. Je ni habari gani njema zilikufanya uamini?

4. Ulipompokea YESU, ni jambo gani Yohana analisema kwenye Yohana 1:12 lilitokea?

(YOHANA 1:12) _____

5. Biblia inasema mliokolewa kwa neema kupitia imani. Neema ni nini?

6. Unaweza kuchukua deni kwaajili ya uzima wa milele?

(WAEFESO 2:8-9) _____

7. Je ulipaswa kusafisha maisha yako ili Mungu akukubali?

(WARUMI 5:8) _____

8. Sasa umemwamini Yesu, je biblia inasema nini kuhusu dhambi zako?

(WAEB 8:12) _____

9. Ukitenda dhambi unatakiwa ufanyeje?

Kuwa mfuasi wa kweli wa Yesu Kristo!

Sasa, kwa kuanzia nataka kusisitiza jambo muhimu sana – umekuwa mkristo kwa muda, mara tu ulipomwamini Yesu Kristo ili akusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele. Lakini, safari ya kukulia kwenye kile Mungu anakihitaji ni furaha ya maisha yako yote. Hii itatokea ukiwa mwanafunzi wa kweli wa Yesu Kristo.

Unaweza kujiuliza, mwanafunzi ni nani? **Ni mtu anayefuata, anayejifunza na kumtii kiongozi.**

Kwenye biblia wafuasi wa Yesu waliitwa wanafunzi.

Na hiki ndicho Mungu anahitaji kwako pia.

Tuliumbwa ili tuwe wanafunzi wa Yesu Kristo.

Kuwa mwanafunzi wa Yesu inajengwa kwa kuwa na mahusiano ya kina na Mungu. Mungu anahitaji maisha yako mapya yajengwe kwa kumjua, kumpenda, kumfurahia kwa sababu ya upendo ulionao kwake, kwa kumtii Yesu Kristo. **Hivi ndivyo utakavyojifunza kuishi kwa amani na furaha. Hivi ndivyo maisha yako yatakavyokuwa na maana na malengo. Hivi ndivyo utakavyopata uzoefu tele na Baraka ya kuwa mkristo. Yote yanatoka kwa Yesu.** Yesu alisema. *“mimi nalikuja ili wawe na*

uzima, kisha wawe nao tele” kuwa mwanafunzi wa Yesu ni heshima kubwa na njia njema ya kuishi. Ningeweza kukueleza sababu elfu za kumfuata Yesu. Lakini zaidi, mwanafunzi humfuata Yesu kwasababu zilezile ambazo wafuasi wake waliweza kumfuata, *“kwasababu yeye ni masihi, mwana wa Mungu aliyehai”* (Math 16:16). Hutajutia kuwa mfuasi wa Yesu!

Roho Mtakatifu; ufunguo wa kuishi na nguvu za Mungu.

Watu wengi watajaribu kukwakwambia funguo za kuishi maisha yenye nguvu ya Yesu ni kufuata sheria nyingi. Watajaribu kukushawishi ukristo ni kujaribu ni mpangilio wa vitu vingi tufanyavyo au tusivyotakiwa kufanya. **HII SIYO. Ukristo ni mahusiano mazuri na MUNGU yanayowezekana kupitia imani ya mwanae (Yesu). Ingawaje hakuna mtu miongoni mwetu kwa nguvu zetu anaweza kuendelea kufanya mambo yote muhimu kuendelea na kufanya mahusiano yaendeleo vizuri. Tunashukuru, Mungu alijua hayo na kutupatia zawadi ya nguvu tutakayohitaji. Zawadi hii ni Roho Mtakatifu wa Mungu.** Yesu anamtambulisha kama msaidizi. *“name nitamwomba baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele”* (YOHANA 14:16). Unaweza kujiuliza huyo Roho Mtakatifu ni nani? Jibu, **Roho Mtakatifu ni roho wa Mungu.** Ukiweka imani yako kwa Yesu, kitu kisicho cha kawaida na kizuri ambacho kitatokea, ni Roho Mtakatifu atakuja kukaa ndani yako.

Sasa, Yesu anahitaji kukupatia uzoefu mkubwa wa Roho Mtakatifu, anahitaji kukubatiza na kukujaza

na Roho Mtakatifu. Yesu akishafanya hivi, **utapokea nguvu na zawadi ya ajabu**, “lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8).

Ni Roho Mtakatifu tu atakayekuwezesha kuishi sawasawa na YESU KRISTO. Ni Roho Mtakatifu utakayemtegemea kukuongoza, kukutia moyo na kukufariji. Ni Roho Mtakatifu atakayeweza kukufundisha biblia na jinsi ya kuomba. Na ni Roho Mtakatifu atakayekuongoza katika huduma ya uponyaji kwa wagonjwa, kuwafungua waliofungwa na kukupa nguvu ya kuwaambia wengine habari za wokovu. Unashngaa? Ni kweli! utaweza kufanya mambo haya yote na mengi kwa kutumia Roho Mtakatifu. Unahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu!

Acha nikueleze unavyoweza kujazwa na Roho Mtakatifu. Yesu alituambia “basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema. Je baba yenu aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?” (Luka 11:13). Kutokana na maelezo ya Yesu kile unachohitaji kufanya ni kumuuliza akubatize kwa Roho Mtakatifu. Acha tumuombe sasa:

Omba maombi haya

“Mpendwa BWANA YESU KRISTO, natamani kujazwa na Roho Mtakatifu ili niwe na nguvu ya kuishi na wewe, ninakuomba unijaze sasa. Nibatize kwa Roho Mtakatifu na nipe uwezo wako ulionao kwangu. Nakushukuru! Ninakutukuza na asante kwa kuitunza ahadi yako kwangu”

ROHO MTAKATIFU: Ufunguo wa kuishi na nguvu za Mungu!

1. Je mwanafunzi ni nani?

2. Kwanini mtua analazimikaika kuwa mwanafunzi wa Yesu?

a. (YOHANA 10:10) _____

b. _____

3. Unahitaji kuwa mwanafunzi wa Yesu?

4. Je ukristo unahusu kufuata sheria nyingi za kufanya ama kutokufanya?

5. Je ni nini msingi wa ukristo?

6. Je tunaweza kuishi kwa nguvu zetu bila kuwa na mahusiano na Mungu?

7. Je Mungu amefanya nini ili kutusaidia?

a. (YOHANA 14:16) _____

b. _____

8. Roho Mtakatifu ni nani?

9. Je Roho Mtakatifu anafanya nini kwako?

a. (MATENDO 1:8) _____

10. Je tunawezaje kujazwa na Roho Mtakatifu?

a. (LUKA 11:13) _____

11. Je umewahi kumpokea Roho Mtakatifu? Kama bado muombe Yesu atubatize sasa na Roho Mtakatifu.

Jinsi ya kuwa imara katika KRISTO

Ili kukua na kuwa mwanafunzi shupavu wa Yesu, jaribu kufikiria juu ya mbegu. Mmea huanza na mbegu. Mbegu huhitaji mambo matatu ili kuweza kukua. Kama hiyo mbegu imepandwa kwenye udongo mzuri, kama imemwagiliwa vizuri na kama inapata mwanga wa kutosha, muujiza utatokea na hiyo mbegu itakuwa na kuwa mmea mkubwa utakaotoa matunda mazuri. Vivyo hivyo, kama vile mbegu, kuna vitu vya msingi utahitaji ili uweze kukua na kuzaa matunda.

Jiunge kwenye kanisa zuri

Kwanza utahitaji upandwe kwenye udongo mzuri. Ndio maana unahitaji kujiunga ndani ya kanisa lililo na nguvu na kutafuta kikundi cha waamini wengine ambao watakusaidia kukua katiak mahusiano mazuri na Yesu. Huwezi ukafanya hivi peke yako; unahitaji msaada wa wengine ambao wako mahili na wameamua kumpenda Yesu. Kupitia msaada wao, utaweza kuimarisha uhusiano wako na Mungu kwa haraka na unaweza kuwasaidia katika upendo wa Mungu pia. Hivyo ndivyo Yesu anavyotaka tuwe. Ametufanya tushirikiane kwa pamoja, kusaidiana na kulindana sisi kwa sisi.



Hata kwenye asili tunaweza kuona mifano ya namna gani tunaweza kuwa kwa pamoja na kuwekana imara na salama.

Bukini ni ndege wakubwa ambao husafiri kwa muda mrefu sana kutafuta chakula kutokana na majira kubadirika. Imeshachunguzwa kuwa hawa bukini huelewa hasa umuhimu wa kukaa kwa pamoja. Kwa mfano kwa kusafiri katika mfumo wa “V”, kundi zima husafiri mala mbili zaidi ya namna ambavyo ndege mmoja angeweza kusafiri akiwa peke yake. Endapo ndege mmoja atajihisi kutoka kwenye mfumo hujikuta anasukumwa na upepo lakini hujiona imara akiona ndege walioko mbele wanasonga. Ndege aliyeko mbele kabisa hufanya kazi ngumu na walioko nyuma hujikuta safari inakuwa ni rahisi kwa. Wakati kiongozi anayeongoza kundi hili anapokuwa amechoka anarudi nyuma, na bukini mwingine atakwenda mbele kuongoza mpaka naye atakapohitaji kupumzika. Na ndege hawa hutiana moyo sana, wakati wanapaa hutoa sauti na kutiana moyo ili kumtia moyo Yule kiongozi awe kwenye mwendo uleule. Mwisho kama bukini ataugua au kujeruhiwa ama kutoka kwenye mfumo wake na kuona kwamba hawezi tena kuendelea na safari bukini wawili hubaki nae ili kumhudumia na kumlinda. Hizi ni kanuni za

kustaajabisha ambazo tunahitaji kuzifuata. Biblia ina tufundisha tena na tena kwamba tunahitajiana.

Kitu kimoja muhimu cha kuwa sehemu ya kanisa ni kwamba, tunachukuliana mizigo. Kama una tatizo ndugu zako katika Kristo watakuchukulia na kukufariji kwa mzigo ulionao. Wagalatia 6:2. Ukipotea njia watakusaidia ili kurejea. Wagalatia 6:1 wewe sasa ni sehemu ya familia ya Mungu na unaihitaji familia yako na familia inakuhitaji wewe. Kanisa ni familia yako mpya.

Katika biblia, neno la la Mungu linasema “chuma hunoa chuma ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki zake” Mithali 27:17. Ukiwa kwenye kikundi cha waamini, tunanoana sisi kwa sisi, ikimaanisha tunasaidiana sisi kwa sisi kuwa imara katika BWANA. Tunasaidiana sisi kwa sisi kwa maswali na matatizo mbalimbali na tunafundishana mambo ambayo Mungu anatumfundisha. Hii ina nguvu sana na ni muhimu kwa kile Mungu anakusudia sisi tuwe.

Faida nyingine ya kuwa sehemu ya kanisa ya waumini wenye nguvu na shauku ni kama bukuni ambao hupaa juu kwenye mfumo mmoja kwa umbali mrefu sana, kwahiyo tunaweza kutimiza mambo mengi sana kama tutafanya kazi kwa pamoja. Walawi 26: 8 inasema “na watu watano wa kwenu watawafukuza watu mia, na watu mia wa kwenu watawafukuza watu elfu kumi”. Hii inamaanisha tukifanya kazi kwa pamoja katika Kristo tunaweza tukakamilisha mara 100 zaidi kama tungejaribu kufanya peke yetu.

Biblia inatuhimiza tuwe sehemu ya kikundi chenye nguvu cha waumini wenye kutia moyo. “wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi

ya wengine: bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadri muonavyo siku ile kuwa inakaribia” (Waebrania 10:25)

Wote tunakumbana na matatizo katika maisha yetu. Hata kama hatujawahi, wote tutapitia hali ya kupoteza ndugu zetu tuwapendao; wote tunaweza kupitia nyakati za kushindwa, matatizo ama kuumizwa. Lakini kama tumeunganishwa kwa upendo wa Yesu, hatutapitia magumu haya peke yetu. Tunapojisikia tuko peke yetu, matatizo yetu yanaonekana ni makubwa na kuogopesha. Lakini kama tuna ndugu ambao wanatujali na kusimama pamoja nasi na kutuomba, kitu kikubwa cha kiimani na kiroho kitatokea. Ni muujiza wa kimaisha. Angalau tunajisikia vizuri. Mizigo yetu huonekana myepesi, na imani yetu inakua. Hii ni kanuni ya muhimu sana kuikumbuka; tunahitajiana! Unahitaji familia ya kanisa. Unahitaji waumini wengine ambao wanakujali na ambao pia unawajali. Huu ndio upendeleo na jukumu letu sote katika familia ya Mungu.

Ubatizo

Mwisho, kanisa zuri ni lile unaweza kubatizwa kwenye maji. Hili ni tendo la muhimu la utii. Inaonyesha kwa namna gani unahitaji kumfuata YESU, miaka 2000 iliyopita baada ya mkutano wa injili wa kwanza, watu 3000 walipokea ujumbe wa injili. Walimuuliza mhubiri je imewapasa kufanya



nini? *“Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja katika jina lake Yesu, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu”* (Matendo 2:38). Sasa umekwisha kutubu na kuamini habari njema za Yesu. Ni ishara kwa ulimwengu kuwa umemfanya Yesu Kristo kuwa BWANA. Tumekwisha kujifunza kuwa tumeokolewa kwa kuamini, hata hivyo, Yesu mwenyewe alituamulu sisi tuliomwamini kubatizwa ndani ya maji. Unatakiwa kukifanya hiki kipaumbele chako kubatizwa haraka iwezekanavyo. Ni uzoefu wa kufurahisha na heri na tendo muhimu la utii kwa Mungu.

Hizi hapa ni ishara zitakazoweza kukutambulisha kanisa zuri la kibiblia

- 1) **Tafuta kanisa lenye furaha.** Hii furaha ni kutoka kwa Roho Mtakatifu na utalifahamu ukisha liona. Ni kanisa ambalo watu wanapendana na wanaofurahi kuonana. Ni watu wanaosalimu wageni na kuonyesha shauku na upendo.
- 2) **Tafuta kanisa linalofundisha biblia na linaamini kuwa biblia ni halisi na hai na kwamba ni neno la Mungu kamili la kutuongoza katika maisha yetu.**
- 3) **Tafuta kanisa lenye dhamira ya utume.** Hili ni, agizo kuu lililotolewa kwa wale wanaomwamini Yesu; *“basi enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe”* (Marko 26:15). Hili ni kanisa linalowafikia waliopotea, maskini na wagonjwa kuwapa tumaini linalopatikana kwenye injili ya Yesu.

- 4) Mwisho, viongozi katika kanisa hilo lazima wawe na sifa ambazo biblia inasema ni muhimu sana kwa wasimamizi (viongozi au wachungaji) wa kanisa. Hapa ndivyo biblia inavyosema:

“Maana imempasa askofu asiwe mtu anayeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu, asiwe mtu wa kujipendeza nafsi zake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu; bali awe mkaribishaji mpenda wema mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kuthibiti nafsi yake; akishika lile neno la imani vilevile, kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga”.

(TITO 1: 7-9)

Hata hivyo, hakuna mmoja wetu aliye kamili na hakuna wachungaji au makanisa kamilifu. Lakini ni muhimu kutafuta kanisa ambalo linajitahidi kuishi kwa heshima, kibiblia na unyenyekevu.



Ushirika/kanisa: Unapaswa kubatizwa na kujiunga na kanisa.

1. Kwanini kuwa sehemu ya kanisa ni kama kupandwa kwenye udongo mzuri?

2. Kwanini mtu angependa kuwa ni sehemu ya kanisa zuri?

a. (WAGALATIA 6:2) _____

b. (WAGALATIA 6:1) _____

c. (MITHALI 27:17) _____

d. (WALAWI 26:8) _____

e. (WAEBRANIA 10:25) _____

3. Ni jambo gani mtume Petro aliwaambia waamini wanya wanapaswa kufanya?

(MATENDO 2:38) _____

4. Je ni mambo gani muhimu katika kutafuta kanisa zuri?

a. _____

b. _____

c. _____

d. (TITO 1:7-9) _____

Jifunze na iishi biblia

Jambo jingine la msingi katika kuona yote ambayo

Mungu anayo kwako ni neno la Mungu, Biblia.

Unajua mbegu, hata kama itapandwa katika udongo mzuri, haiwezi kukua labda imepokea maji mengi

ya kutosha. Vivyo hivyo wewe huwezi kukua kama Mungu alivyokufanya uwe bila kumwagiliwa na maji ya neno la Mungu.

Biblia ni kitabu cha ajabu sana kuwahi kuandikwa, **ni mkusanyiko wa vitabu 66, chenye vitabu na barua, vyote viliandikwa na wanadamu waliopewa uvuvio kutoka kwa Mungu “kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki”** (2 Timotheo 3:16). Vitabu hivi vilihifadhiwa kwa miujiza kutoka kwenye lugha zake za asili kwa miaka maelfu. Biblia imetafisiliwa kwenye karibu kila lugha iliyopo hapa ulimwenguni. Na Biblia ni kitabu kilichosomwa zaidi, kilichofundishwa sana, kilicho chapishwa sana na kitabu chenye ushawishi katika maisha ya wanadamu.

Kitabu hiki cha kushangaza cha Mungu, kimeonyesha kila maada ya maisha yetu na kinatoa ushauri kamili wa Mungu kwa kila hali tunayopitia. Biblia inatufundisha juu ya Mungu, jinsi alivyo na nini kilicho cha muhimu kwake. Pia inatufundisha kuhusu sisi wenyewe. Biblia inasema kwamba ulipofanyika mkristo umekuwa kiumbe kipya. Mungu anatuambia kupitia Biblia kuwa tumekuwaje na nguvu ya kushangaza ambayo ipo kwetu tunavyoendelea kujifunza na kutembea kwa imani.

Jambo la muhimu kuelewa kuhusu Biblia ni kwamba, Biblia si kama vitabu vingine hapa duniani. **Kimeandikwa kutokana na neno harisi la Mungu;** kwahiyo ina nguvu kuliko vitabu vyote vilivyowahi kuandikwa. Biblia ina nguvu ya kufanya imani yetu

iweze kukua *“imani huja kwa kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo”* (Warumi 10:17). **Hii inamaanisha kwamba unapolisoma, na kujifunza na kufikiria juu ya neno la Mungu, imani yako hakika itakua. Biblia pia itakufundisha jinsi ya kuwa mzazi, rafiki ama mchumba mwenye hofu ya Mungu. Itakufundisha jinsi ya kufanikiwa kwenye biashara, kwenye familia yako na katika mahusiano yako na Mungu. Biblia itakufundisha namna ya kuishi.**

Ingawaje Biblia, ingeweza kuitwa kitabu kilichofungwa. **Hii inamaanisha kwa uhakika kuelewa na kubadirishwa na neno la Mungu, Mungu mwenyewe anafungua akiri zetu ili tuweze kuelewa.** Wakati mwingi mtu asiyeamini hujaribu kuielewa Biblia kwa sababu ya uongo na anashindwa kupokea kile Mungu anazungumza. Na bado mtu anayempenda Mungu anaweza kupokea vingi kutoka kwenye biblia kuliko mtu mahili ambaye hana imani. Hata wanafunzi wa Yesu waliokuwa naye kwa miaka mitatu, walimhitaji Yesu ili afungue akiri zao ili kuyaelewa maandiko. *“ndipo alipowafunulia akiri zao wapate kuelewa na maandiko”* (Luka 24:45) hii ndiyo inapaswa iwe hata kwako. Roho Mtakatifu atakayekuongoza kwenye maisha yako yote, ndiye hasa atakufunulia akiri zako kuelewa maana ya neno la Mungu. **Kwahiyo kila muda unapofungua neno la Mungu, kabla hata hujaanza kulisoma, chukua**

muda wa kumweleza Mungu azungumze na wewe kupitia neno lake. Utashangazwa kwa utofauti, kama utasoma kwa mtazamo wa unyenyekevu na hamu ya kufundishwa na Mungu.

Kama hauna biblia au hauna uwezo wa kuisoma, mtafute mtu anayeweza kuisoma na msome kwa pamoja. **Kama una biblia chukua muda kila siku kuisoma na kujifunza.** Kama unamfahamu mtu asiyeweza kuisoma au asiyekuwa nayo, unaweza kuwaalika mkasoma kwa pamoja. Na usiwe na haraka. Jaribu kufikiria unachokisoma na namna utakavyoweza kutumia katika maisha yako. Mruhusu Yesu azungumze na roho yako na akubadirishe kadri unavyojifunza mambo ambayo ni kweli, sawa na haki. Usihofu kupigia msitari aya ambazo utaona zinazungumza na wewe. Andika maswali unapokutana na kitu usichokielewa, ili umuulize mtu anayeweza kukupa majibu. Biblia ilitolewa na Mungu kwasababu anakupenda na anahitaji ufanikiwe kila sehemu ya maisha yako. Si kwamba tu Biblia itakufundisha jinsi ya kuishi, lakini itakubadirisha kiimani kutoka ndani hadi nje.

Sasa nataka nikupe zawadi ya dhahabu ambayo itakusaidia kila siku ya maisha yako. Je uko tayari kwa hilo? Hii hapa. Roho Mtakatifu ambaye sasa anaishi kwako atakupa nguvu ya kuwa mtu anayefanyia kazi neno la Mungu, siyo kama msikilizaji tu au msomaji



tu. Watu wengi sana wanapenda kuisoma Biblia lakini hawapendi kukiishi kile biblia inachosema. Usiruhusu wewe mwenyewe uangukie kwenye mtego si vizuri ujue kweli ya Mungu lakini usiifuate. Tunakua tunapokuwa watu wa kuuishi ukweli huu. Hii ndiyo siri ya kuishi na furaha ambayo Mungu anayo kwako. Hii ndiyo siri ya kuwa na nguvu na hekima ya Roho Mtakatifu. Hii kanuni rahisi itakusaidia kuwa utakua na kufanya yale yote Mungu aliyokuwekea. Hata sasa ninakushawishi uombe maombi haya:-

“Mpendwa baba wa mbinguni, asante kwa kunipa neema ya kuwa mtendaji wa neno. Nifanye mtu wa kukuamini wewe na kuishi kwa ujasiri kama usemavyo. Nikumbushe na nitie nguvu kufanya yale yote ambayo neno lako linanifundisha kufanya, ninachagua kuwa mtu ambaye si msikilizaji tu bali mtendaji wa neno usemalo, ninakushukuru kwa neema yako kufanya hivi, ninaomba katika jina la Yesu Kristo aliye BWANA na mwokozi wangu” amina.

SOMO LA 4

BIBLIA:

1. Ni nani aliandika biblia?

2. Kwanini biblia ni tofauti na vitabu vinginne?

(2 TIMOTHEO 3:16) _____

3. Nini kinatokea unaposoma na kuisikiliza biblia?

(WARUMI 10:17) _____

4. Ni mambo ya aina gani ambayo Biblia itatufundisha?

5. Je ungependa kujifunza Biblia?

6. Inamaanisha nini kusema Biblia ni kitabu kilichofungwa?

(LUKA 24:45) _____

7. Kabla hujaanza kuisoma biblia ni jambo gani la Msingi unapaswa kufanya kwanza?

(YOHANA 10:27) _____

8. Ni mara ngapi utafanikiwa ukiisoma Biblia?

Ushirika na Mungu kwenye maombi

Tumekuwa tukifananisha ukuaji wa maisha ya kikristo na mbegu ambyo inaleta mmea kamili ambao huzalisha matunda. Sisi ni mbegu, kanisa ni udongo neno la Mungu ni maji na mwisho maombi yanaweza kuwa jua linaloongezeka katika uwepo wa Mungu.

Maombi ni kitu rahisi sana: ni kuwasiliana

na Mungu. Ni kuongea na Mungu lakini pia ni kusikiliza kile anachokuambia. Jambo la kustaajabisha kuhusu maombi ni kwamba muumbaji wa ulimwengu, **Mungu mmoja, Mungu muweza, ana hamu sana kuzungumza na wewe. Anahitaji umfahamishe kila sehemu ya maisha yako, na anahitaji uweze kumjua yeye.**

Maombi ni njia tuanyoweza kuleta wasiwasi

wetu au mashaka kwa Mungu. Ni namna tunavyoleta mahitaji yetu na haja zetu kwake.

Maombi ni njia ya moja kwa moja ya kuzungumza na Mungu. Na muunganiko huu ni muhimu ndio maana biblia inatueleza kuomba bila kukoma. Biblia inasema “*msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu zijulikane na Mungu*”. (Wafilipi 4:6). Hii inamaanisha tunaendelea kuzungumza na kuwasiliana na Mungu ambaye ni baba yetu. Maombi yetu yanaweza kuzungumzwa kwa sauti ama kimya kimya. Yanaweza kufanywa kwa kupiga magoti, tukiwa tumekaa, tumesimama, tukitembea, tukikimbia, tukiendesha au muda wowote au mahali popote tunapojikuta. Hakuna muda au mahali ambapo Mungu hataki uache kuwa naye shirika kwenye maombi. Maombi yako hayahitajiki kuwa na mpangilio au fasaha. Yanatakiwa kuwa ya kipekee na kutoka ndani ya moyo wako.

Maombi yana nguvu!

Maombi yanabadiri mambo mbalimbali, biblia inatuambia kuwa kuna nguvu kubwa kwenye maombi na yana ahadi nyingi zenye ufanisi kutoka kwa Mungu. Katika Biblia Yakobo 5:16b inasema “*kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii*”. Yesu mwenyewe alisema “*kwasababu hiyo nawaambia yoyote myaombayo aminini kuwa mnayapokea nayo yatakuwa yenu*” (Marko 11:24). Katika msitali huu tunaona jambo moja la muhimu sana ni kuamini! **Tunapaswa kuamini kuwa Mungu amesikia na atajibu maombi yetu.**

Jambo jingine la msingi kutambua wakati

tuaomba ni kuomba mambo ambayo yako katika mapenzi ya Mungu. Wakati mwingine, sababu inayotufanya tusipokee tukiombacho ni kwa sababu tunaombo yale ambayo Mungu hapendezwi nayo kwetu. “*Na huu ndio ujasili tulionao kwake, ya kuwa tukiomba sawasawa na mapenzi yake atusikia; na kama tukijua kwamba atusikia tuombacho chote, twajua kuwa tunazo zile haja tulizomwomba*” (1 Yohana 5:14-15). Njia ya kutambua kama maombi yako yako katika mapenzi ya Mungu ni kuomba mambo ambayo biblia inasema Mungu anahitaji. Hakikisha kwamba unatilia maanani na pia usiache kumwambia Mungu mahitaji yako katika sala.

Ninakushauri kwamba si kwamba tu uendelee kuzungumza na Mungu lakini kwamba tenga muda maalumu wa kuongea na Mungu kila siku. Hapa ni mfano mdogo utakaokusaidia kuanza

- **SIFU**
- **SHUKURU**
- **OMBA**
- **SIKILIZA**

SIFU: mshukuru Mungu kwa jinsi alivyo na kile alichokufanyia. Tazama angani na jaribu kufikiri kuwa ndiye aliyeumba jua, mwezi na nyota. Angalia juu ya vitu asili na mshukuru Mungu kwa namna

Maombi ni rahisi sana, ni kuwasiliana na Mungu.



alivyotupatia kila kitu tunacho kihitaji duniani. Fikiria kwa habari ya msalaba ambao Yesu alitoa maisha yake na msifu Mungu kwa kukuokoa kutoka dhambini. Roho yako imtukuze Mungu wetu alivyo wa ajabu na kumsifu kwa hilo.

SHUKURU: Mshukuru Mungu kutoka rohoni mwako. Tenga muda wako ukimshukuru Mungu kwa kila kitu ulichonacho kwenye maisha yako. Mshukuru Mungu kwa vitu vya kawaida ulivyonavyo kama mavazi, chakula mezani pako. Mshukuru kwa pumzi uliyonayo kwenye mapafu yako na akiri yako. Jifunze kutengeneza tabia ya mfululizo katika kumshukuru Mungu. Mungu ni mzuri na ni wa neema sana kwetu na tunapaswa kila mara kuweka kwenye akiri zetu. Uwe mtu wa kumshukuru Mungu kila wakati. *“shukuruni kwa kila jambo maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu”* (1 Wathesalonike 5:18). Mtazamo huu utajenga imani yako na kukujaza amani na furaha.

OMBA: Leta kwa Mungu mahitaji yako yote. Muombe Mungu ombea familia na marafiki. Muombe Mungu afya njema na nguvu. Muombe Mungu akupe mwongozo kwenye maisha yako. Muulize Mungu kwa kila kitu kilicho ndani ya moyo wako. Kumbuka anakupenda na anatamani kukupa vitu vizuri. Biblia inasema kwamba *“hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni nanyi mtapata, furaha yenu iwe timilifu”* (Yohana 16:24). Mungu hawezi kuwa na wazimu kwa wewe kumuomba.

SIKILIZA: Tenga muda Fulani kwa ajili ya kusikiliza tu, na sikiliza kile Roho Mtakatifu atazungumza na wewe. Atazungumza na wewe kupitia Biblia, lakini

pia atazungumza na wewe ndani ya moyo wako. Inaweza isije kama sauti lakini kama mawazo au hisia ambazo utaelewa bila maneno. Hivyo ndivyo mungu anavyo kuongoza kukupa uelekeo wa maisha. Yesu anasema *“kondoo wangu waisikia sauti yangu, nami nawajua, nao wanifuata”* (Yohana 10:27). Hata hivyo kama vile unavyoweza kutafuta mawimbi ya sauti katika redio ndivyo tunavyotakiwa kutafuta sauti ya Mungu. Hii itachukua vitendo, lakini, hapo tutakapofanya, furaha na hekima inayokuja kutokana na kusikia neno la Mungu ni ya ajabu sana kuliko maneno yanavyoweza kueleza. Kama unavyojifunza kuisikiliza sauti ya Mungu, kumbuka, Mungu hawezi kukwambia kitu kinachopingana na biblia.

Ukweli ni kwamba faida za maombi ni nyingi sana kuweza kuhesabiwa na hakuna nafasi hata katika kitabu hiki kuwe kuziandika zote. Lakini kama utakavyojitoa mwenyewe kwenye maombi, utagundua hazina ya maombi kwa mara ya kwanza.

Rafiki yangu faida za maombi ni nyingi sana hazihesabiki, na hakuna nafasi ya kuweza kuziandika zote katika hiki kitabu. Lakini kama utakavyojitoa mwenyewe kwenye maombi utagundua faida yako ya maombi.

SOMO LA 5

Maombi:

1. Jadili inawezekanaje sala iwe kama kuteleza kwenye jua.

2. Maombi ni nini?

3. Je Mungu anahitaji kuzungumza na wewe?

4. Je ni sehemu gani ya maisha yako Mungu anaipenda sana?

5. Badala ya kuwa na wasiwasi , tunaweza kuombea nini?

(WAFILIP 4:6) _____

6. Ni mahari gani tunaweza kumuomba Mungu?

(WAEFESO 6:16) _____

7. Je Mungu anasema nini kuhusu nguvu ya maombi?

(YAKOBO 5:16) _____

8. Ni jambo gani la muhimu kwetu kutegemea majibu kutoka kwenye maombi yetu?

(MARKO 11:24) _____

9. Nini kinatupa ujasiri kwamba BWANA atajibu maombi yetu?

(1 YOHANA 5:14-15) _____

10. Ni mambo gani ya kufanya kwenye maombi?

a. MSIFU MUNGU: _____

b. MSHUKURU MUNGU: (1 WATHESALONIKE 5:18) _____

c. MUOMBE MUNGU: (YOHANA 16:24) _____

d. SIKILIZA: (YOHANA 10:27) _____

11. Hatua inayofuata:

12. Ni hatua gani inafuata katika kukua kwenye mahusiano yako na Mungu?

13. Unakwenda kuhakikishaje kwamba moto huu haufi au kuwa baridi?

Mawazo ya mwisho

Kama ninavyojiandaa kukuaga sasa, ninataka nikwambie tena jinsi Mungu anavyokupenda. Ana maisha yaliyojaa utajili wa upendo, furaha na amani atakupa kusudi na uelekeo na sababu na atakufanya ukue katika hekima, nguvu na neema. Mfuatilie kwa moyo wako wote. Maamuzi uliyoyafanya katika kuamini na kumwamini Yesu ilikuwa ni mwanzo tu. Mungu amekuandalia vitu vingi sana kuliko unavyoweza kutarajia. Mpende Yesu kwa moyo wote, kwa nafsi yako yote na kwa akiri yako yote na kwa nguvu zako zote na hutajutia siku zote za maisha yako.

Mungu akutunze na kukubariki. Mungu akulinde na na kukukuza katika kila kizuri na cha kustaajabu. Ambacho alikuumbia wewe uwe.

Ni mimi rafiki na kaka katika Yesu Kristo BWANA wetu.



Ev. Dr. Dana Morey

Leo nimempokea Yesu kuwa
BWANA na mwokozi wa maisha
yangu nilipochukua maamuzi ya
kumwamini yeye, kusamehe dhambi
zangu na kunifanya kiumbe kipya.
Nimesamehewa na sasa ni mwana wa
Mungu!

Imesainiwa _____

Tarehe _____



aLn

A Light to the Nations

KADI YA MAAMUZI

Jina: _____

Umri: _____ Me ☐ Ke ☐

Mahali unapoishi: (andika taarifa maalumu) _____

Namba ya simu: _____

Je ni mala ya kwanza kumwamini Yesu? Ndio ☐ Hapana ☐

Je unahitaji kuja kutembelewa? Ndio ☐ Hapana ☐

Je ni muda gani kuja kukutembelea? _____

Kwa maelezo zaidi jinsi ya kukua katika maisha yako mapya na Kristo, tembelea Tovuti yetu katika **www.alttn.com**. Hapo pia utakuta toleo jipya la kitabu hiki kwa njia ya sauti katika lugha mbalimbali na zana zingine za Biblia.

Pia unaweza kutupata kwenye facebook katika:

A Light to the Nations

Na

Evangelist Dana Morey



Ev. Dr. Dana Morey

www.alighttothenations.com